

Song 4 – Natamani kuwa malaika

Artists: Lady Jay Dee

Language Swahili

Video URL

<http://www.youtube.com/watch?v=Q86OsvZF0QY>

Maana ya maneno (Words and Expressions Explained)

Natamani- I wish

Malaika-angel

Kurudi nyuma – to go back

Moyo-heart

Theluji-snow

Chuki-hatred

Tabasamu-smile

Adui-enemy

Bili- bills

Kubembelezwa-soothe

Kubezwa- to be ignored

Kubeba-carry

Katu-never

Adha-problems

Majukumu-responsibilities

Nisingefikiria-I would not have thought

Kufikiri-to think

Muda ninaoamua-time that I decide

Majaribu- difficulties in life

Machungu- bitterness

Kuhisia/kuhisi- feel

Raha- comfort

Mzigo- burden

Jalala - dumpsite

Masuali (Questions)

1. Mwimbaji anatamani kuwa nani? Kwanini? Toa sababu mbili.
2. Kama mwimbaji asikuwa mkubwa, ni vitu gani asingevipata? Sema vitu viwili.
3. Je mwandishi anaamini kuwa ukubwa ni raha? Kwanini?
4. Kwanini unafikiri anasema ukubwa ni jalala?
5. Mwimbaji anasema kuna tofauti gani kati ya zamani na sasa wakati anapolia?
6. Kwanini anasema moyo wake ni mweupe kama theluji?

Mazoezi (Exercise)

1. Sikiliza nyimbo kwa makini na andika maneno ambayo yanakosekana (Listen to the song carefully and find the missing words)

Verse 1

Natamani kuwa _____

Natamani tena _____

Natamani kuwa kama _____

Natamani kuwa kama _____

_____ wangu _____ kama theluji

Si _____ mabaya wala _____ duniani ooh

_____ hata kwa _____ kuishi bila kulipa _____

Nikilia _____ si sasa nabezwa

Nikichoka tembea _____, kila kitu mimi _____

Malaika, mtoto ni malaika.

Verse 2

Natamani kuwa _____

Natamani tena _____

Natamani kuwa kama _____

Natamani kuwa kama _____

Kama mimi _____ mkubwa

Katu _____ za dunia

_____ nisingefikiria kulala muda _____

“stress” zisingenifika, _____ nisingepata

_____ nisingehisia

Kama hii leo _____, natamani kuwa malaika

Kiitikio

Verse 3

Mnasema ukubwa _____

Lakini _____ mkubwa

Ukubwa _____ .

Kiitikio

2. Andika kwa ufupi useme nyimbo hii inazungumzia nini?
3. Andika hadithi ya kuelezea kinachozungumzwa katika nyimbo hii.
4. Jee wewe unatamani vitu kama anavyotamani mwimbaji? Jee una sababu gani?
5. Unafikiri nini maana ya malaika katika nyimbo hii? Jee hapa marekani maana hii ya malaika ipo?
6. Elezea maisha ya kulipa bili hapa Marekani na ingekuwaje kama watu wangeishi bila kulipa bili?
7. Kitu gani kinamfanya mtu mmoja ambeze mtu mwingine?
8. Jee unakubaliana na mwimbaji anaposema kuwa ukubwa ni jalala? Kwanini?
9. Andika sentensi zenye maana kwa kutumia maneno yafuatayo. Kila sentensi isipungue maneno 15:

- (i) Chuki
- (ii) Tabasamu
- (iii) Bili
- (iv) Kubembeleza/kubembeleza
- (v) Kubezwa
- (vi) Kubeba
- (vii) Majukumu

10. Andika sentensi fupi zenye maana kwa kutumia maneno yafuatayo.

- (i) Nisingefikiria
- (ii) Kufikiri
- (iii) Muda ninaoamua
- (iv) Kuhisi
- (v) Raha
- (vi) Mzigo